

**TANGAZO**  
**KONGAMANO LA NNE LA**  
**MTANDAO WA ULIMWENGU WA DINI KWA AJILI YA WATOTO**  
**(GNRC)**

**Dar es Salaam tarehe 16 hadi 18 Juni 2012.**

Tunapenda kutangazia umma wa Watanzania na Ulimwengu kwamba Kongamano la nne la MTANDAO WA ULIMWENGU WA DINI KWA AJILI YA WATOTO (GNRC) utafanyika Dar es Salaam tarehe 16 hadi 18 Juni 2012. Hii ni mara ya kwanza kwa kongamano hili kufanyika nje ya Japan na Ulaya.

Ikumbukwe kwamba tarehe 16 Juni ni siku ya 'Mtoto wa Afrika', kuadhimisha kumbukumbu ya mwaka 1976, mamia ya watoto kule Afrika ya Kusini bila silaha yo yote walipokabiliana na majeshi ya ubaguzi wa rangi na wengi wao wakauawa kukatili wakidai kupata elimu bora na maisha ya heshima.

Dima ya kongamao hili ni: KUMALIZA UMASKINI, KUTAJIRISHA WATOTO: KUTIA MOYO, KUTENDA NA KULETA MABADILIKO.

GNRC ndio mtandao wa pekee wa ushirikiano wa madhehebu makubwa ya dini duniani unaojikita katika kuimarisha haki za watoto na kuwaleta maisha bora.

Wanachama wanatoka katika dini zote kubwa ulimwenguni wakiunganishwa na adhima ya kushirikiana kutengeneza dunia ambapo mtoto ataishi kwa amani na kukuza vipaji vyake.

Kongamano itakuwa na wajumbe 300 wakiwemo wawakilishi toka Umoja wa Mataifa na taasisi zake; Umoja wa Afrika na taasisi shirikishi, watoto na viongozi wa dini toka ulimwenguni kote wakiwemo Wa-bahai, Waislamu, Wabudhisti, Wakristu, Wahindu, Imani za jadi, Washinto na Wayahudi.

Kabla ya kongamano kuu patakuwepo na siku mbili 13-14 Juni 2012 za kongamano ya watoto ili waweke sawa mawazo yao yatakayowasilishwa katika kongamano kuu.

Kongamano itahamasisha utajiri wa dini mbali mbali kwa pamoja bila kuingilia imani ya mtu, kushirikiana kupigana na umaskini kwa watoto kimaadili, kiroho na kijamii. Kushirikiana na wadau wengine kuondoa sababu kuu za umaskini zikiwa:

- Rushwa na utawala mbaya
- Vita na unyanyasaji
- Mgawano usio wa haki wa rasilimali zilizopo.

Mwishoni mwa kongamano tunategemea kwamba kwa adhma ya GNRC juu ya wema wa watoto, sote tuwe tumeadhimi na kuwa kitu kimoja katika kuunga mkono azimio la umoja wa mataifa no. 12 ya Haki ya Mtoto kwamba ni jukumu la kimaadili kwamba mototo ye yote asiishi katika umaskini mkubwa. Na hivyo

- Kuleta mawazo na mahitaji yao mbele kuitia mazungumzano kati yao, na pamoja na viongozi wa dini, viongozi wa siasa na jamii.
- Kuonyesha uwezo wao wa kushiriki katika utekelezaji wakishirikiana na wakubwa
- Wajisikie kama wawajibakaji wenye uelewa katika ngazi ya kimataifa.
- Kuwatia moyo na kuwawezesha kuleta maongeano na elimu ya pamoja katika jamii wanamoishi.

Mwishoni tunategemea kutakuwepo na azimio la kufanya kazi dhidi ya umaskini ikitokana na majadiliano yatakayokuwa yemefanywa yakijikita katika maadili ya ulimwengu. Patakuwepo vile vile na ahadi ya viongozi wa dini kutumia mapokeo ya madhehebu yao na jumuiya zao kupiganana umaskini wakiunganika pamoja katika KUTENDA, KUTAJIRISHA NA KUTIA MOYO WA MABADILIKO.

ASANTE